# Kushiriki Habari za Mtoto
# Child Information Sharing

Swahili | Kiswahili

## Je, kwa nini unataka kushirikisha habari zangu?

**Kutunza watoto wa Victoria**

Ili kuwasaidia watoto wote wa Victoria kuishi maisha salama na yenye furaha, Serikali ya Victoria inaboresha jinsi taarifa inavyoshirikiwa na wataalamu fulani wanaofanya kazi na watoto.

Huduma nyingi tayari zinashirikisha taarifa za mtu. Mpango wa Kushirikisha Habari za Mtoto (Child Information Sharing Scheme [CISS]) huwarahisishia wataalamu hawa kuona picha kamili ya mtoto wanaofanya naye kazi, kuwasaidia kuelewa wanachoweza kushirikisha na jinsi ya kulinda faragha ya familia.

### Je, inasaidiaje familia?

Watoto wengi watahitaji usaidizi katika hatua fulani ya maisha yao. Kuanzia wanapozaliwa, hadi wanapofikisha miaka 18, Marekebisho ya Kushirikisha Habari za Mtoto huwasaidia watoto na familia zao kupata usaidizi bora kutoka kwa wataalamu na mashirika.

### Je, inasaidiaje wataalamu?

Kushirikisha Habari za Mtoto huwawezesha wataalamu wanaowasaidia na kuwatunza watoto (kama vile walimu na wauguzi) kushirikisha ujuzi wao kuhusu mtoto wao kwa wao, huku pia wakitoa miongozo kuhusu nini cha kushirikisha, na jinsi ya kulinda faragha ya familia.

### Mfano:



Taj amehamia shule hivi karibuni. Mwalimu wake mpya, Neema, anaona kwamba anasitasita kuongea darasani, na anatatizika kumaliza kazi yake ya shule. Kwa kuomba taarifa kutoka kwa shule ya awali ya Taj, Neema anajifunza kwamba ana dyslexia, ambayo humfanya asisite kushiriki akiwa darasani.

**Huu ni mfano wa habari ambayo yanaweza kushirikishwa kupitia Kushiriki Habari za Mtoto, kwani humruhusu mwalimu wa Taj kuunda mpango wa somo unaosaidia mahitaji ya kujifunza ya Taj.**

# Je, unaishirikisha na nani? Je, itatumikaje?

## Aina ya habari iliyoshirikishwa

Taarifa yoyote ambayo inasaidia ustawi au usalama wa watoto inaweza kushirikishwa. Hii inaweza kuwa taarifa kama vile usaidizi wa kitaaluma ambao mtoto anapokea, au maarifa kuhusu mahusiano ya familia.

**Je, taarifa inatumika kwa nini**

- **Kuhakikisha kuwa hautahitaji kueleza habari zako mara mbili**
- **Kuhusisha watu sahihi ambao wanaweza kusaidia**
- **Kuona picha kamili**
- **Kuwasaidia watoto kustawi**

## Je, nani anaweza kushiriki na kupata taarifa?

Ni watu fulani pekee ndio wana mamlaka ya kushirikishwa taarifa - siyo kila mtu. Watu hawa ni wataalamu ambao wana wajibu wa kutunza na kulinda watoto, kama vile walimu, madaktari, wafanyakazi wa kijamii na washauri, wauguzi na polisi.



## Mfano:

Lisa ni muuguzi wa shule ambaye amekuwa akifanya kazi na Alice, na binti yake mwenye umri wa miaka mitano, Jasmine, ambaye ana ugonjwa mdogo wa moyo. Kwa kuwa Jasmine anaanza shule ya msingi, Lisa anazungumza na Alice, na kutafuta maoni yake kuhusu kushirikisha taarifa kuhusu hali ya Jasmine na muuguzi wa shule yake ya msingi, ili kuhakikisha kwamba wanafahamu mahitaji yake. Lisa anafahamu maoni ya Alice kabla ya kushiriki habari hiyo.

**Huu ni mfano wa wakati mtaalamu anaweza kuchagua kushiriki habari, na mtu ambaye anaweza kushiriki naye.**

# Je, habari inaweza kushirikishwa lini?

## Habari haiwezi kushirikishwa isipokuwa:

1. **Itatumika kukuza ustawi au usalama wa mtoto (au kikundi cha watoto).**
2. **Kushiriki kutasaidia katika kutoa huduma, kupanga mipango au kuchunguza au kudhibiti hatari kwa watoto.**
3. **Haitahatarisha mtu yeyote, kupigwa marufuku kisheria au kutengwa chini ya kanuni.**

Kwa orodha kamili ya masharti ambayo lazima yatimizwe kabla ya habari kushirikishwa, tembelea www.infosharing.vic.gov.au

## Je, taarifa inashirikishwa namna gani?

Mashirika na wataalamu walioidhinishwa kisheria wanaweza kuomba habari au kuamua kuyashiriki.

## Kuweka habari kwa faragha na salama

Sehemu ya kuwalinda watoto ni kuhakikisha taarifa zao pia zinawekwa salama. Kushiriki Habari za Mtoto kunaunga mkono sheria zilizopo za faragha kwa kuwaambia wataalamu wakati wanapoweza kushirikisha habari chini ya sheria hizo. Ni kosa kushiriki habari za siri wakati hazihitajiki. Pamoja na hayo, taarifa zote lazima zihifadhiwe kwa usalama na mashirika binafsi. Mafunzo hutolewa kwa wafanyakazi hao walioidhinishwa, hivyo wanafahamu wajibu wao.

## Mfano:

Andy ni mfanyakazi wa usaidizi wa kijamii ambaye anapokea ombi kutoka kwa afisa wa uandikishaji wa shule ya upili kushiriki habari kuhusu Lee. Andy alisaidia familia ya Lee wakati hawakuwa na makazi kwa muda mfupi. Baada ya kushauriana na Lee na familia yake, Andy haishiriki habari kuhusu hali yao ya maisha, kwa kuwa anashuku kuwa inaweza kutumika kumtenga Lee asijiandikishe katika shule hiyo.

**Huu ni mfano ambapo wataalamu hawawezi kushiriki habari - afisa wa uandikishaji si mtaalamu aliyeidhinishwa, na habari hayatumiki kusaidia ustawi au usalama wa Lee au familia yake.**

# Malalamiko

## Iwapo una wasiwasi kuwa habari yanaweza kuwa yameshirikisha kwa njia ambayo hairuhusiwi, una haki ya kutoa maoni na kulalamika

**Ili kulalamika kwa mara ya kwanza, zungumza na shirika lililoshirikisha taarifa hiyo. Mashirika yote yanapaswa kuwa na taratibu za kushughulikia malalamiko.**



## Ikiwa haujaridhika kuwa suala hilo limetatuliwa, malalamiko yanaweza kufanywa kwa:

**Ofisi ya Kamishna wa Habari wa Victoria ikiwa malalamiko yanahusu habari za kibinafsi**

Tovuti: ovic.vic.gov.au / Simu: 1300 666 444

**Kamishna wa Malalamiko ya Afya ikiwa malalamiko yanahusu taarifa za afya**

Tovuti: hcc.vic.gov.au / Simu: 1300 582 113

## Ikiwa ungependa maelezo zaidi kuhusu Mpango wa Kushiriki Habari za Mtoto unaweza:

**Tupige simu:** 1800 549 646

**Tuandikie:** CISandFVIS@education.vic.gov.au

**Tembelea tovuti:** vic.gov.au/child-information-sharing-scheme